ISSN 0856 - 034X

THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA

***Supplement No. 19*** ***17th May, 2024***

***SUBSIDIARY LEGISLATION***

*To The Gazette of the United Republic of Tanzania No. 20 Vol. 105 Dated 17th May, 2024*
Printed by The Government Printer, Dodoma by Order of Government

TANGAZO LA SERIKALI NA. 389 la tarehe 17/05/2024

SHERIA YA UCHAGUZI WA RAIS, WABUNGE NA MADIWANI,
(NA. 1 YA MWAKA 2024)

# KANUNI

*(Zimetengenezwa chini ya kifungu cha 161)*

KANUNI ZA UBORESHAJI WA DAFTARI LA KUDUMU LA WAPIGA KURA ZA MWAKA 2024

MPANGILIO WA KANUNI

*Kanuni* *Jina*

SEHEMU YA KWANZA
MASHARTI YA UTANGULIZI

1. Jina.
2. Matumizi.
3. Tafsiri.

SEHEMU YA PILI
KUANZISHWA KWA KATA

4. Kata.
5. Kata kuwa eneo la uchaguzi.
6. Kubadili mipaka ya eneo la uchaguzi.

SEHEMU YA TATU
UTEUZI WA WATENDAJI WA UANDIKISHAJI

7. Uteuzi wa mratibu wa uandikishaji wa mkoa.
8. Maafisa waandikishaji.
9. Uteuzi wa maafisa waandikishaji wasaidizi.
10. Kiapo cha kutunza siri na tamko.
11. Uteuzi wa mwandishi msaidizi na mwendeshaji wa kifaa cha bayometriki.
12. Taratibu na sifa za uteuzi wa waandishi wasaidizi na waendeshaji wa vifaa vya bayometriki.
13. Mafunzo kwa watendaji wa uandikishaji.

SEHEMU YA NNE
UBORESHAJI WA DAFTARI LA KUDUMU LA WAPIGA KURA

14. Mahali na muda wa kuboresha Daftari.
15. Kuanzishwa kwa vituo vya uandikishaji.
16. Uandikishaji wa wapiga kura kwenye vituo.
17. Mawakala wa uandikishaji.
18. Kutokuwepo kwa wakala katika kituo cha uandikishaji.
19. Wanaoruhusiwa kuingia kwenye vituo vya uandikishaji.
20. Sifa za kuandikishwa.
21. Maombi ya kuandikishwa.
22. Kadi ya mpiga kura.
23. Kukataliwa kuandikishwa.
24. Marekebisho ya taarifa.
25. Kuhamisha taarifa za uandikishaji.
26. Kubadilisha kadi ya mpiga kura iliyopotea, kuharibika au kufutika.
27. Utaratibu wa kuanzisha mchakato wa uboreshaji wa taarifa kwa njia ya kielektroniki.
28. Kufutwa kwa majina kwenye Daftari.
29. Kufutwa kwa kadi ya mpiga kura.
30. Uwasilishaji wa taarifa zilizoboreshwa na fomu kwa afisa mwandikishaji.
31. Maandalizi ya Daftari la Awali la Wapiga Kura.
32. Taarifa za Daftari la Awali la Wapiga Kura.
33. Kuwasilisha Daftari la Awali la Wapiga Kura kwa maafisa waandikishaji.
34. Uwekaji wazi wa Daftari la Awali la Wapiga Kura.

*Tangazo la Serikali Na. 389 (Linaendelea.)*


35. Marekebisho ya taarifa za mpiga kura.
36. Kukosekana kwa majina katika Daftari la Awali la Wapiga Kura.

SEHEMU YA TANO
PINGAMIZI NA RUFAA

37. Pingamizi dhidi ya wapiga kura walioandikishwa.
38. Rufaa.
39. Kuwasilisha taarifa zilizoboreshwa kwa Mkurugenzi wa Uchaguzi.

SEHEMU YA SITA
DAFTARI LA KUDUMU LA WAPIGA KURA NA UTHIBITISHO

40. Maandalizi ya Daftari.
41. Uthibitisho wa Daftari.
42. Kuwasilisha Daftari la Kudumu la Wapiga Kura.
43. Utoaji wa Daftari la Kudumu la Wapiga Kura kwa vyama vya siasa.
44. Kuingiza, kurekebisha na kubadili taarifa katika Daftari.

SEHEMU YA SABA
USHIRIKIANO KATIKA MATUMIZI YA VIFAA NA TAARIFA

45. Makubaliano ya kutumia vifaa na taarifa.

SEHEMU YA NANE WAANGALIZI
WA UANDIKISHAJI

46. Mwaliko na usajili wa waangalizi.
47. Muda wa uangalizi.
48. Taarifa na maelezo kwa waangalizi.
49. Haki na wajibu wa waangalizi.
50. Kukosa sifa ya kuwa waangalizi.
51. Taarifa ya waangalizi wa uandikishaji.

SEHEMU YA TISA
MAKOSA NA ADHABU

52. Makosa yanayofanywa na watendaji wa uandikishaji.
53. Kughushi, kufuta au kuharibu taarifa.

54. Kumiliki nyaraka za kughushi.
55. Taarifa za uongo.
56. Kukaidi kuondoka katika eneo la uandikishaji.
57. Uchapishaji na uharibifu usioruhusiwa.
58. Adhabu.

SEHEMU YA KUMI
MASHARTI MENGINEYO

59. Kurejesha kadi ya mpiga kura aliyefariki.
60. Uchapishaji wa notisi.
61. Kufutwa kwa Kanuni.

---

MAJEDWALI

---

OFISI YA MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI TANZANIA
WELEDI NA UBORA
PROFESSIONALISM & EXCELLENCE
THE OFFICE OF THE ATTORNEY GENERAL TANZANIA

*Tangazo la Serikali Na. 389 (Linaendelea.)*

SHERIA YA UCHAGUZI WA RAIS, WABUNGE NA MADIWANI,
(NA. 1 YA MWAKA 2024)

## KANUNI

*(Zimetengenezwa chini ya kifungu cha 161)*

KANUNI ZA UBORESHAJI WA DAFTARI LA KUDUMU LA WAPIGA KURA ZA MWAKA 2024

### SEHEMU YA KWANZA
### MASHARTI YA UTANGULIZI

Jina

**1**. Kanuni hizi zitajulikana kama Kanuni za Uboreshaji wa Daftari la Kudumu la Wapiga Kura za Mwaka 2024.

Matumizi

**2.** Kanuni hizi zitatumika katika uboreshaji wa Daftari la Kudumu la Wapiga Kura.

Tafsiri

**3.** Katika Kanuni hizi, isipokuwa kama muktadha utahitaji vinginevyo-

"afisa mwandikishaji" maana yake ni mtu aliyeteuliwa chini ya kifungu cha 7 cha Sheria na inajumuisha afisa mwandikishaji msaidizi;

"afisa wa Tume" maana yake ni mwajiriwa wa Tume;

Sura ya 258

"chama cha siasa" maana yake ni chama cha siasa kilichosajiliwa chini ya Sheria ya Vyama vya Siasa;

"Daftari" maana yake ni Daftari la Kudumu la Wapiga Kura lililoanzishwa chini ya kifungu cha 12 cha Sheria;

"Daftari la Awali la Wapiga Kura" maana yake ni daftari lililoanzishwa chini ya kifungu cha 11 cha Sheria;

"jimbo" maana yake ni jimbo la uchaguzi kwa madhumuni ya uchaguzi wa Mbunge;

"kadi ya mpiga kura" maana yake ni kadi inayotolewa kwa mujibu wa Sheria, ikithibitisha kwamba mtu aliyetajwa katika kadi hiyo ameandikishwa kuwa

mpiga kura;

Sura ya 287 na 288

"kata" maana yake ni mgawanyo wa mamlaka katika mamlaka za serikali za mitaa kwa mujibu wa masharti ya Sheria ya Serikali za Mitaa (Mamlaka za Wilaya) na Sheria ya Serikali za Mitaa (Mamlaka za Miji);

Sura ya 2

"Katiba" maana yake ni Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977;

"kiapo cha kutunza siri" maana yake ni kiapo kinachozuia kutoa taarifa yoyote ya mtu aliyeomba kuandikishwa au jambo lolote linalohusu uandikishaji isipokuwa kwa madhumuni yaliyoidhinishwa kwa mujibu wa sheria;

Sura ya 287

"kijiji" itakuwa na maana sawa kama ilivyotafsiriwa katika Sheria ya Serikali za Mitaa (Mamlaka za Wilaya);

Sura ya 287

"kitongoji" itakuwa na maana sawa kama ilivyotafsiriwa katika Sheria ya Serikali za Mitaa (Mamlaka za Wilaya);

"kituo cha uandikishaji" maana yake ni kituo kilichoanzishwa na Tume kwa ajili ya kuandikisha wapiga kura;

Sura ya 58

"mfungwa" itakuwa na maana sawa kama ilivyotafsiriwa katika Sheria ya Magereza na kwa madhumuni ya Kanuni hizi, inajumuisha mahabusu;

Sheria Na. 2 ya Mwaka 2024

"Mkurugenzi wa Uchaguzi" itakuwa na maana sawa kama ilivyotafsiriwa katika Sheria ya Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi;

Sura ya 288

"mtaa" itakuwa na maana sawa kama ilivyotafsiriwa katika Sheria ya Serikali za Mitaa (Mamlaka za Miji);

"mwangalizi wa uandikishaji" maana yake ni mwangalizi wa uandikishaji wa ndani au wa kimataifa aliyeidhinishwa na Tume;

"mwandishi msaidizi" maana yake ni mtu aliyeteuliwa na afisa mwandikishaji chini ya kanuni ya 11 na itajumuisha mwendeshaji wa kifaa cha bayometriki;

"namba ya kipekee ya utambuzi wa mpiga kura" maana yake ni namba ya kudumu ya utambulisho wa

mpiga kura;

Sheria Na. 1 ya Mwaka 2024

"Sheria" maana yake ni Sheria ya Uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani;

"taarifa za uandikishaji" maana yake ni taarifa za mpiga kura zilizoandaliwa kwa mujibu wa masharti ya Sheria;

"Tume" maana yake ni Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi;

"uboreshaji" maana yake ni uandikishaji wa wapiga kura wapya wenye sifa, ufanyaji wa marekebisho ya taarifa za wapiga kura, uhamishaji wa taarifa za wapiga kura, utoaji wa kadi mpya kwa wapiga kura na ufutaji wa majina ya waliopoteza sifa kwenye Daftari;

"uchaguzi" maana yake-

(a) iwapo ni kumchagua Rais, ni uchaguzi wa Rais;

(b) iwapo ni kumchagua Mbunge, ni uchaguzi wa Mbunge, na inajumuisha uchaguzi mdogo; na

(c) iwapo ni kumchagua Diwani, ni uchaguzi wa Diwani, na inajumuisha uchaguzi mdogo;

"vifaa vya uandikishaji" maana yake ni vifaa vilivyopata kibali cha Tume kwa lengo la kutumika katika uandikishaji;

"wakala wa uandikishaji" maana yake ni mtu aliyeteuliwa na chama cha siasa kuwa wakala chini ya kifungu cha 17 cha Sheria; na

"watendaji wa uandikishaji" inajumuisha mratibu wa uandikishaji wa mkoa, afisa mwandikishaji, afisa mwandikishaji msaidizi, mwandishi msaidizi, mwendeshaji wa kifaa cha bayometriki na watendaji wengine watakaoteuliwa na Tume.

## SEHEMU YA PILI
## KUANZISHWA KWA KATA

Kata
Sura ya 287 na 288

**4.-**(1) Kata zitaanzishwa kwa mujibu wa masharti ya Sheria ya Serikali za Mitaa (Mamlaka za Wilaya) na Sheria ya Serikali za Mitaa (Mamlaka za Miji).

(2) Endapo Waziri mwenye dhamana ya Serikali za Mitaa ataanzisha kata kwa mujibu wa Sheria ya

Serikali za Mitaa (Mamlaka za Wilaya) na Sheria ya Serikali za Mitaa (Mamlaka za Miji), kata hiyo itakuwa ni kata kwa madhumuni ya uchaguzi wa madiwani chini ya Sheria.

Kata kuwa eneo la uchaguzi

**5.** Kwa kuzingatia masharti ya kanuni ya 4, Tume itatumia kata kama eneo la uchaguzi.

Kubadili mipaka ya eneo la uchaguzi

**6.-**(1) Tume inaweza kubadili mipaka ya maeneo ya uchaguzi pale yatakapotokea mazingira yatakayoathiri mipaka iliyopo ya maeneo ya uchaguzi.

(2) Mazingira yanayoweza kuathiri mipaka iliyopo ya maeneo ya uchaguzi yatajumuisha-

(a) kuanzishwa kwa mkoa, eneo la kiutawala la wilaya, halmashauri, kata, kijiji au mtaa;
(b) kubadilishwa kwa mipaka ya mkoa iliyopo, eneo la kiutawala la wilaya, halmashauri, kata, kijiji au mtaa; au
(c) kufutwa kwa mkoa, eneo la kiutawala la wilaya, halmashauri, kata, kijiji au mtaa.

## SEHEMU YA TATU
## UTEUZI WA WATENDAJI WA UANDIKISHAJI

Uteuzi wa waratibu wa uandikishaji wa mikoa

**7.**-(1) Kwa kuzingatia masharti ya kifungu cha 7(2) cha Sheria, Tume itateua mratibu wa uandikishaji wa mkoa kutoka miongoni mwa watumishi wa umma.

(2) Bila kuathiri masharti ya kanuni ndogo ya (1), kwa upande wa Tanzania Zanzibar, Tume itateua waratibu wawili wa uandikishaji, mmoja kwa ajili ya mikoa ya Unguja na mwingine kwa ajili ya mikoa ya Pemba.

(3) Kwa madhumuni ya kanuni ndogo ya (1) na (2), mratibu wa uandikishaji wa mkoa atapewa barua ya uteuzi ambayo itaainisha-

(a) majukumu;
(b) tarehe ya kuanza utekelezaji wa majukumu;
(c) muda wa kuhudumu;
(d) vigezo na masharti ya utekelezaji wa majukumu; na
(e) maelekezo mengine kadri Tume au

Mkurugenzi wa Uchaguzi atakavyoona inafaa.

(4) Mratibu wa uandikishaji wa mkoa aliyeteuliwa ataitaarifu Tume kwa maandishi kuhusu kukubali uteuzi ndani ya siku kumi na nne baada ya kupokea barua ya uteuzi.

(5) Endapo mratibu wa uandikishaji wa mkoa, bila sababu ya msingi, atashindwa kutekeleza matakwa ya kanuni ndogo ya (4), Tume itateua mtu mwingine kuwa mratibu wa uandikishaji wa mkoa.

(6) Mratibu wa uandikishaji wa mkoa aliyeteuliwa kwa mujibu wa Kanuni hizi atawajibika -

(a) kuratibu uendeshaji wa zoezi la uboreshaji ndani ya mkoa;
(b) kuhakikisha upatikanaji wa vifaa vya uboreshaji na rasilimali nyingine;
(c) kuratibu taarifa; na
(d) kuchukua hatua nyingine muhimu ili kufanikisha uboreshaji wa Daftari.

(7) Mratibu wa uandikishaji wa mkoa aliyeteuliwa chini ya kanuni hii atatekeleza majukumu yake chini ya usimamizi wa Tume.

Maafisa waandikishaji

**8**.-(1) Afisa mwandikishaji aliyerejewa katika kifungu cha 7(1) cha Sheria atawajibika kusimamia na kuratibu uendeshaji wa uboreshaji wa Daftari.

(2) Bila kujali masharti ya kanuni ndogo ya (1), pale ambapo mazingira yatahitaji na kwa kuzingatia masharti ya Sheria, Tume inaweza kuteua mtu mwingine yeyote miongoni mwa watumishi wa umma kuwa afisa mwandikishaji.

(3) Afisa mwandikishaji aliyeteuliwa atapewa barua ya uteuzi ambayo itaainisha-

(a) majukumu;
(b) tarehe ya kuanza utekelezaji wa majukumu;
(c) masharti na vigezo vya utekelezaji wa majukumu;
(d) muda wa kuhudumu;
(e) utaratibu na namna uboreshaji wa Daftari utakavyofanyika; na
(f) maelekezo mengine kadri Tume au

Mkurugenzi wa Uchaguzi atakavyoona inafaa.

(4) Afisa mwandikishaji aliyeteuliwa chini ya kanuni hii ataitaarifu Tume kwa maandishi kuhusu kukubali uteuzi ndani ya siku kumi na nne baada ya kupokea barua ya uteuzi.

(5) Afisa mwandikishaji atatekeleza majukumu yake chini ya usimamizi wa Tume.

Uteuzi wa maafisa waandikishaji wasaidizi

**9.**-(1) Kwa kuzingatia masharti ya kifungu cha 7(2) cha Sheria, Tume inaweza kuteua afisa mwandikishaji msaidizi kutoka miongoni mwa watumishi wa umma.

(2) Afisa mwandikishaji msaidizi atapewa barua ya uteuzi ambayo itaainisha-

(a) majukumu;

(b) tarehe ya kuanza utekelezaji wa majukumu;

(c) masharti na vigezo vya utekelezaji wa majukumu;

(d) muda wa kuhudumu; na

(e) maelekezo mengine yoyote kama itakavyoamuliwa na Tume au Mkurugenzi wa Uchaguzi.

(3) Afisa mwandikishaji msaidizi aliyeteuliwa ataitaarifu Tume kwa maandishi kuhusu kukubali uteuzi ndani ya siku kumi na nne baada ya kupokea barua ya uteuzi.

(4) Endapo afisa mwandikishaji msaidizi aliyeteuliwa atashindwa kuzingatia kanuni ndogo ya (3) bila sababu ya msingi, Tume itamteua afisa mwingine wa umma kuwa afisa mwandikishaji msaidizi.

(5) Afisa mwandikishaji msaidizi aliyeteuliwa chini ya kanuni hii, atatekeleza majukumu yake chini ya usimamizi wa afisa mwandikishaji.

Kiapo cha kutunza siri na tamko

**10.** Kabla ya kuanza utekelezaji wa majukumu, mratibu wa uandikishaji wa mkoa, afisa mwandikishaji au afisa mwandikishaji msaidizi-

(a) atatoa tamko la kujitoa uanachama au kutokuwa mwanachama wa chama cha siasa

mbele ya Hakimu kwa kutumia Fomu Na. 6 iliyoainishwa katika Jedwali la Kwanza; na

(b) ataapa kiapo cha kutunza siri mbele ya Hakimu kwa kutumia Fomu Na. 7 iliyoainishwa katika Jedwali la Kwanza.

Uteuzi wa mwandishi msaidizi na mwendeshaji wa kifaa cha bayometriki

**11.**-(1) Kwa madhumuni ya uboreshaji wa Daftari na kwa kuzingatia masharti ya Sheria na maelekezo ya Mkurugenzi wa Uchaguzi, kila afisa mwandikishaji atateua kwa maandishi mwandishi msaidizi, mwendeshaji wa kifaa cha bayometriki au mtendaji mwingine yeyote kwa kila kituo cha uandikishaji.

(2) Mwandishi msaidizi aliyeteuliwa katika kanuni ndogo ya (1) atakuwa kiongozi wa kituo na iwapo kituo kitakuwa na mwandishi msaidizi zaidi ya mmoja, afisa mwandikishaji atateua kiongozi wa kituo kutoka miongoni mwa waandishi wasaidizi.

(3) Kiongozi wa kituo atakuwa msimamizi na mtoa uamuzi wa mwisho katika shughuli zote zinazohusu uandikishaji wa wapiga kura katika kituo cha uandikishaji.

(4) Tume itaamua idadi ya waandishi wasaidizi na waendeshaji wa vifaa vya bayometriki wanaohitajika katika kila kituo cha uandikishaji.

(5) Mtu yeyote aliyeteuliwa chini ya kanuni hii atapaswa kusaini mkataba wa ajira na afisa mwandikishaji katika Fomu Na. 4 iliyoainishwa katika Jedwali la Kwanza.

(6) Kwa kuzingatia masharti ya Sheria na maelekezo yatakayotolewa na Tume au Mkurugenzi wa Uchaguzi, mwandishi msaidizi, mwendeshaji wa kifaa cha bayometriki au mtendaji mwingine yeyote aliyeteuliwa chini ya kanuni ndogo ya (1), atatekeleza majukumu yake chini ya usimamizi wa afisa mwandikishaji au afisa mwandikishaji msaidizi.

Taratibu na sifa za uteuzi wa waandishi wasaidizi na waendeshaji

**12.**-(1) Wakati wa kuteua waandishi wasaidizi na waendeshaji wa vifaa vya bayometriki, afisa mwandikishaji -

(a) atatangaza nafasi za kazi ili kuwaalika watu

wa vifaa vya bayometriki

wenye sifa kuwasilisha maombi kwa kuzingatia sifa zilizoanishwa katika kanuni ndogo ya (2);

(b) atabandika orodha ya majina ya waombaji waliochaguliwa kwa ajili ya usaili katika ofisi ya afisa mwandikishaji au kwenye ofisi yoyote ya umma iliyopo ndani ya eneo la uchaguzi;

(c) atawasaili waombaji;

(d) atachagua waombaji waliofaulu usaili mapema iwezekanavyo mara baada ya usaili;

(e) atabandika majina na kuwataarifu kwa maandishi waombaji waliochaguliwa; na

(f) atasaini mkataba wa ajira na waombaji waliochaguliwa kwa kutumia Fomu Na. 4 iliyoainishwa katika Jedwali la Kwanza.

(2) Kwa madhumuni ya kanuni ndogo ya (1)(a), mtu anaweza kuteuliwa kuwa mwandishi msaidizi au mwendeshaji wa kifaa cha bayometriki ikiwa atakuwa na sifa zifuatazo:

(a) ni raia wa Tanzania;

(b) ametimiza umri wa miaka kumi na nane;

(c) amehitimu elimu ya kidato cha nne au zaidi na anajua kusoma na kuandika katika lugha ya Kiswahili au Kiingereza;

(d) ni mkazi wa kata au shehia anayoomba kuwa mwandishi msaidizi au mwendeshaji wa kifaa cha bayometriki;

(e) si kiongozi au kada wa chama cha siasa; na

(f) ni mwadilifu na mtiifu.

(3) Kabla ya kuanza utekelezaji wa majukumu, mwandishi msaidizi au mwendeshaji wa kifaa cha bayometriki-

(a) atatoa tamko la kujitoa uanachama au kutokuwa mwanachama wa chama cha siasa mbele ya afisa mwandikishaji au afisa mwandikishaji msaidizi kwa kutumia Fomu Na. 6 iliyoainishwa katika Jedwali la Kwanza; na

(b) ataapa kiapo cha kutunza siri mbele ya afisa mwandikishaji au afisa mwandikishaji

msaidizi kwa kutumia Fomu Na. 7 iliyoainishwa katika Jedwali la Kwanza.

(4) Bila kujali masharti ya kanuni ndogo ya (2)(d), Tume inaweza kutoa maelekezo kwa afisa mwandikishaji kuteua mtu mwingine yeyote kuwa mwandishi msaidizi au mwendeshaji wa kifaa cha bayometriki kadri itakavyoonekana ni muhimu.

Mafunzo kwa watendaji wa uandikishaji

**13.** Wakati wowote baada ya kuteua watendaji wa uandikishaji na kabla ya kuanza uboreshaji wa Daftari, Tume itaandaa na kutoa mafunzo kuhusu sheria, taratibu na mchakato wa uboreshaji kwa watendaji wa uandikishaji.

## SEHEMU YA NNE
## UBORESHAJI WA DAFTARI LA KUDUMU LA WAPIGA KURA

Mahali na muda wa kuboresha Daftari

**14.-**(1) Uboreshaji wa Daftari utafanyika katika vituo vya uandikishaji wa wapiga kura katika jimbo au kata kwa muda ambao Tume itapanga.

(2) Uboreshaji wa Daftari unaweza kufanyika katika jimbo au kata mbalimbali kwa nyakati tofauti kadri Tume itakavyopanga.

(3) Tume inaweza kuongeza muda wa kuboresha Daftari katika jimbo au kata ikiwa itaonekana ni muhimu.

Kuanzishwa kwa vituo vya uandikishaji

**15.-**(1) Kwa madhumuni ya kuboresha Daftari ndani ya jimbo au kata, na kwa kuzingatia masharti ya Sheria na maelekezo yatakayotolewa na Tume, kila afisa mwandikishaji ataanzisha-

(a) angalau kituo kimoja cha uandikishaji katika kila mtaa au kijiji; na

(b) ikiwa ni mamlaka ya mji mdogo, kituo cha uandikishaji katika baadhi ya vitongoji kama itakavyoamuliwa.

(2) Kituo cha uandikishaji kitaanzishwa katika-

(a) majengo ya umma;

(b) maeneo ya wazi na yanayoweza kufikika na watu wote; au

(c) magereza au vyuo vya mafunzo kwa ajili ya

wafungwa na wanafunzi wa vyuo vya mafunzo kwa kuzingatia masharti yaliyoanishwa katika Jedwali la Pili.

(3) Kwa kuzingatia masharti ya kanuni ndogo ya (2), vituo vya uandikishaji havitaanzishwa katika-

(a) kambi za jeshi;

(b) vituo na kambi za polisi;

(c) maeneo ya ibada; au

(d) majengo au ofisi za vyama vya siasa.

(4) Bila kujali masharti ya kanuni ndogo ya (2), Tume au Mkurugenzi wa Uchaguzi anaweza kutoa maelekezo kwa afisa mwandikishaji kuanzisha kituo cha uandikishaji katika sehemu ambayo hakuna majengo ya umma.

(5) Vituo vya uandikishaji vilivyoanzishwa na afisa mwandikishaji vinaweza kutumiwa na taasisi nyingine za Serikali baada ya kushauriana na Tume.

Uandikishaji wa wapiga kura kwenye vituo

**16**. (1) Kwa kuzingatia masharti ya Sheria na Kanuni hizi, mwandishi msaidizi ataandikisha wapiga kura kwa ajili ya kuboresha Daftari katika kituo cha uandikishaji ndani ya jimbo au kata.

(2) Kwa kuzingatia masharti ya kifungu cha 10(1)(c) cha Sheria, utaratibu wa kuwaandikisha wafungwa au wanafunzi wa vyuo vya mafunzo na mahabusu wenye sifa ya kuwa wapiga kura utakuwa kama ulivyoanishwa katika Jedwali la Pili.

Mawakala wa uandikishaji

**17.-**(1) Chama cha siasa kinaweza kuteua mtu mmoja kwa kila kituo cha uandikishaji kuwa wakala wa uandikishaji na kuwasilisha taarifa kwa Tume kuhusu uteuzi huo kwa mujibu wa kifungu cha 17 cha Sheria.

(2) Taarifa kuhusu uteuzi wa wakala itaambatishwa na-

(a) picha mbili za rangi zenye ukubwa sawa na picha ya pasi ya kusafiria;

(b) nakala ya kitambulisho cha taifa, leseni ya udereva, kadi ya mpiga kura au pasi ya kusafiria.

(3) Wakati wa kuwasilisha taarifa kuhusu uteuzi

wa mawakala chini ya kanuni ndogo ya (1), chama cha siasa kinaweza kuwasilisha majina ya mawakala mbadala kwa kila kata kwa idadi ambayo Tume itaelekeza.

(4) Kabla ya kuanza kutekeleza majukumu, wakala wa uandikishaji au wakala mbadala wa uandikishaji ataapa kiapo cha kutunza siri mbele ya afisa mwandikishaji au afisa mwandikishaji msaidizi siku saba kabla ya kuanza zoezi la uboreshaji au ndani ya kipindi kifupi kama Tume itakavyoruhusu kwa kutumia Fomu Na. 7 iliyoainishwa katika Jedwali la Kwanza.

Kutokuwepo kwa wakala katika kituo cha uandikishaji

**18.** Kwa kuzingatia masharti ya Kanuni hizi, ikiwa kitendo au shughuli yoyote inatakiwa kuthibitishwa au kufanywa mbele ya wakala wa uandikishaji, kutokuwepo kwa wakala huyo kwa muda na sehemu iliyopangwa kwa ajili hiyo, hakutabatilisha kitendo au shughuli hiyo iwapo imefanywa kwa mujibu wa Sheria.

Wanaoruhusiwa kuingia kwenye vituo vya uandikishaji

**19.** Mtu yeyote hataruhusiwa kuingia katika kituo cha uandikishaji isipokuwa wafuatao:

(a) mwandishi msaidizi;
(b) mwendeshaji wa kifaa cha bayometriki;
(c) mpiga kura au mtu anayeomba kuandikishwa;
(d) wakala wa uandikishaji;
(e) afisa mwandikishaji;
(f) afisa mwandikishaji msaidizi;
(g) mratibu wa uandikishaji wa mkoa;
(h) Mjumbe wa Tume;
(i) Mkurugenzi wa Uchaguzi;
(j) afisa wa Tume;
(k) afisa wa taasisi nyingine ya Serikali aliyeidhinishwa na Tume;
(l) afisa anayeshughulikia uchaguzi;
(m) mwangalizi aliyeidhinishwa na Tume; na
(n) mtu mwingine yeyote aliyeidhinishwa na Tume

Sifa za kuandikishwa

**20**. Mtu atakuwa na sifa za kuandikishwa iwapo-

(a) ni raia wa Tanzania;
(b) ametimiza umri wa miaka kumi na nane;

OFISI YA MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI TANZANIA
THE OFFICE OF THE ATTORNEY GENERAL TANZANIA

(c) hajaondolewa sifa za kuandikishwa na sheria yoyote;
(d) atatimiza umri wa miaka kumi na nane kabla au ifikapo siku ya uchaguzi;
(e) ni mkazi wa kawaida katika jimbo au kata ambayo anaomba kuandikishwa;
(f) ana akili timamu;
(g) hajatiwa hatiani kwa kosa ambalo adhabu yake ni kifo au hatumikii kifungo kwa kosa ambalo adhabu yake inazidi miezi sita;
(h) hajawekwa kizuizini kwa amri ya Rais; na
(i) hana utii wa nchi nyingine tofauti na Tanzania.

Maombi ya kuandikishwa

**21.**-(1) Mtu yeyote mwenye sifa ya kuandikishwa kuwa mpiga kura anaweza kuwasilisha maombi kwa mwandishi msaidizi kwa lengo la kuandikishwa ndani ya muda ulioelekezwa wa uboreshaji wa Daftari katika eneo la uchaguzi.

(2) Endapo mwandishi msaidizi atajiridhisha kuwa mwombaji ana sifa za kuandikishwa kuwa mpiga kura, atamwandikisha mwombaji kupitia Fomu Na.1 iliyoainishwa katika Jedwali la Kwanza kisha, mwombaji atachukuliwa alama za vidole, picha na saini.

(3) Endapo mtu anaomba kuandikishwa kuwa mpiga kura na ikiwa kumbukumbu na taarifa zake zinazohusu kuandikishwa zinaweza kupatikana kutoka kwenye kanzidata ya taasisi ya Serikali inayohusika na uandikishaji au usajili na utambuzi wa watu, Tume inaweza kutumia kumbukumbu na taarifa hizo kwa ajili ya kumwandikisha mwombaji.

(4) Kwa kuzingatia kanuni ndogo ya (2) na (3), baada ya kuandikishwa, mwombaji atapewa kadi ya mpiga kura.

(5) Mwandishi msaidizi atajaza sehemu inayoonesha majumuisho ya idadi ya Fomu Na. 1 zilizotumika kwa siku husika katika Fomu Na. 2 iliyoainishwa katika Jedwali la Kwanza.

Kadi ya mpiga kura

**22.** Kadi ya mpiga kura itakuwa na taarifa zifuatazo:

(a) jina kamili;
(b) picha;
(c) tarehe ya kuzaliwa;
(d) jinsi;
(e) namba ya kipekee ya utambuzi wa mpiga kura;
(f) jina la kituo cha uandikishaji;
(g) msimbo wa haraka wa utambuzi;
(h) alama za usalama;
(i) saini ya Mkurugenzi wa Uchaguzi;
(j) saini ya mpiga kura; na
(k) taarifa nyingine yoyote kama Tume itakavyoelekeza.

Kukataliwa kuandikishwa

**23.-**(1) Mwandishi msaidizi anaweza kukataa kumwandikisha mwombaji iwapo ataridhika kuwa mwombaji hana sifa za kuandikishwa kuwa mpiga kura.

(2) Endapo mwandishi msaidizi atakataa kumwandikisha mwombaji chini ya kanuni ndogo ya (1) na ikiwa mwombaji atahitaji, mapema inavyowezekana, atapaswa kumueleza sababu za kukataa kumwandikisha kwa kujaza Fomu Na. 3A iliyoainishwa katika Jedwali la Kwanza.

(3) Ndani ya siku saba baada ya kupokea sababu ya kukataliwa, mwombaji ambaye hataridhika na uamuzi wa mwandishi msaidizi anaweza kuwasilisha kwa afisa mwandikishaji Fomu Na. 3A iliyojazwa kwa ajili ya mapitio ya uamuzi wa mwandishi msaidizi.

(4) Afisa mwandikishaji atatoa uamuzi wa maombi ya mapitio ndani ya siku kumi na nne baada ya kupokea maombi hayo.

(5) Baada ya kupokea Fomu Na. 3A iliyojazwa ipasavyo, afisa mwandikishaji ataamua iwapo mwombaji ana sifa au hana sifa za kuandikishwa kama mpiga kura na kumfahamisha mwombaji ipasavyo.

(6) Mwombaji ambaye hataridhika na uamuzi wa afisa mwandikishaji anaweza kukata rufaa Mahakama ya Mwanzo ndani ya siku kumi na nne baada ya uamuzi kutolewa.

(7) Mahakama ya Mwanzo itatoa uamuzi wa rufaa ndani ya siku kumi na nne tangu siku rufaa

ilipowasilishwa.

(8) Uamuzi wa Mahakama ya Mwanzo utakuwa ni wa mwisho.

Marekebisho ya taarifa

**24.-**(1) Endapo taarifa katika kadi ya mpiga kura au Daftari zinahitaji kufanyiwa marekebisho kwa sababu ya kubadilika kwa jina au mabadiliko mengine yoyote katika mazingira ambayo yatamuathiri mtu mwenye kadi ya mpiga kura, mtu anaweza kuomba kwa mwandishi msaidizi kurekebisha taarifa.

(2) Endapo mwandishi msaidizi atajiridhisha kuwa taarifa za mwombaji zinapaswa kurekebishwa-

(a) atamtaka mpiga kura kurudisha kadi ya mpiga kura; na

(b) atamwandikisha mwombaji kwa kutumia Fomu Na. 5A iliyoainishwa katika Jedwali la Kwanza na atampa mwombaji kadi nyingine yenye namba ya kipekee ya utambuzi wa mpiga kura inayofanana na iliyopo katika kadi ya awali.

(3) Bila kuathiri kanuni ndogo ya (2), kadi mpya ya mpiga kura haitatolewa hadi mwombaji-

(a) atakapowasilisha nyaraka inayotambulika kwa mujibu wa sheria, endapo ni mabadiliko ya jina; na

(b) atakapomthibitishia afisa mwandikishaji, mwandishi msaidizi au mtendaji mwingine yeyote kama itakavyoelekezwa na Tume kwa madhumuni ya uandikishaji wa wapiga kura kuwa kadi hiyo imepotea au imeharibika.

(4) Endapo mwombaji atashindwa kurudisha kadi ya mpiga kura kutokana na sababu kwamba kadi imepotea au kuharibika, mwombaji atatoa tamko la kisheria kwa kutumia Fomu Na. 5A iliyoainishwa katika Jedwali la Kwanza

(5) Endapo mwandishi msaidizi atamwandikisha mwombaji chini ya kanuni hii atajaza sehemu inayoonesha majumuisho ya idadi ya Fomu Na. 5A zilizotumika kwa siku husika katika Fomu Na. 2 iliyoainishwa katika Jedwali la Kwanza.

Kuhamisha taarifa za uandikishaji

**25**.-(1) Mtu aliyeandikishwa kama mpiga kura katika eneo moja la uchaguzi, ambaye amehama na kuwa mkazi wa kawaida katika eneo lingine la uchaguzi, anaweza kuomba kwa mwandishi msaidizi kuhamisha taarifa zake kwenda katika eneo la uchaguzi alilohamia.

(2) Mwandishi msaidizi ambaye maombi yamewasilishwa kwake, iwapo ataridhika kwamba mwombaji anaishi katika eneo la uchaguzi ambalo maombi yamefanyika na bado ana sifa za kuandikishwa kuwa mpiga kura, atamtaka mwombaji kuwasilisha kwake kadi ya mpiga kura na ikiwa kadi imepotea au kuharibika atamtaka kutoa tamko na atamwandikisha katika Fomu Na. 5A iliyoainishwa katika Jedwali la Kwanza na kumpa kadi mpya yenye namba ya kipekee ya utambuzi wa mpiga kura inayofanana na iliyopo katika kadi ya awali.

(3) Endapo mwandishi msaidizi atamwandikisha mwombaji chini ya kanuni hii, atajaza sehemu inayoonesha majumuisho ya idadi ya Fomu Na. 5A zilizotumika kwa siku husika katika Fomu Na. 2 iliyoainishwa katika Jedwali la Kwanza.

Kubadilisha kadi ya mpiga kura iliyopotea, kuharibika au kufutika

**26.-**(1) Endapo kadi ya mpiga kura iliyotolewa kwa mtu imepotea, imefutika au kuharibika mtu huyo anaweza kutoa taarifa kwa mwandishi msaidizi.

(2) Kwa kuzingatia kanuni ndogo ya (1), iwapo mwandishi msaidizi atajiridhisha na mazingira ya kupotea, kufutika au kuharibika kwa kadi ya mpiga kura-

(a) atamtaka mtu huyo kutoa tamko la kisheria katika Fomu Na. 5A iliyoainishwa katika Jedwali la Kwanza;

(b) atakamilisha kujaza Fomu Na. 5A iliyoainishwa katika Jedwali la Kwanza na atampa mpiga kura kadi mpya yenye namba ya kipekee ya utambuzi wa mpiga kura inayofanana na iliyopo katika kadi ya awali; na

(c) atajaza sehemu inayoonesha majumuisho ya idadi ya Fomu Na. 5A zilizotumika kwa siku husika katika Fomu Na. 2 iliyoainishwa katika Jedwali la Kwanza.

Utaratibu wa kuanzisha mchakato wa uboreshaji wa taarifa kwa njia ya kielektroniki

**27.** Kwa madhumuni ya kanuni ya 24 na 25, mpiga kura anaweza kuanzisha mchakato wa awali kwa njia ya kielektroniki ili kurekebisha au kuhamisha taarifa zake katika Daftari kutoka kituo cha awali kwenda kituo kingine.

Kufutwa kwa majina kwenye Daftari

**28.-**(1) Mpiga kura anaweza kutoa taarifa kwa mwandishi msaidizi, kuhusu mtu au watu ambao wamepoteza sifa za kuwa kwenye Daftari.

(2) Kwa kuzingatia kanuni ndogo ya (1), mwandishi msaidizi atamtaka mpiga kura kujaza Fomu Na. 5B iliyoainishwa katika Jedwali la Kwanza.

(3) Baada ya kujaza fomu chini ya kanuni ndogo (2), mwandishi msaidizi atapaswa-

(a) kumtaka mpiga kura kurejesha kadi ya mtu aliyepoteza sifa ya kuwepo katika Daftari ikiwa anayo; na

(b) kuwasilisha Fomu Na. 5B na Fomu Na. 2 kwa afisa mwandikishaji.

(4) Kwa ajili ya ufanisi wa uboreshaji wa Daftari, Tume inaweza kutumia kumbukumbu za wapiga kura waliofariki kutoka kwenye taasisi ya Serikali inayojihusisha na usajili wa vifo, kwa madhumuni ya kufuta majina yao katika Daftari.

(5) Endapo taarifa imepatikana kutoka kwenye taasisi ya Serikali chini ya kanuni ndogo ya (4), Fomu Na. 5B haitajazwa.

(6) Endapo mwandishi msaidizi atapokea taarifa chini ya kanuni hii, atajaza sehemu inayoonesha majumuisho ya idadi ya Fomu Na. 5B zilizotumika kwa siku husika katika Fomu Na. 2 iliyoainishwa katika Jedwali la Kwanza.

Kufutwa kwa kadi ya mpiga kura

**29.-**(1) Kadi yoyote ya mpiga kura ambayo imepotea, imeharibika au kufutika, ambayo inatakiwa kurejeshwa chini ya Kanuni hizi, itachukuliwa kama imefutwa.

(2) Endapo kadi ya mpiga kura iliyopotea imepatikana baada ya muda wa uandikishaji, itapaswa

kurejeshwa Tume.

Uwasilishaji wa taarifa zilizoboreshwa na fomu kwa afisa mwandikishaji

**30.-**(1) Baada ya kukamilisha zoezi la uboreshaji wa Daftari katika kituo cha uandikishaji kwenye eneo la uchaguzi, mwandishi msaidizi atawasilisha taarifa zilizoboreshwa na fomu kwa afisa mwandikishaji au afisa mwandikishaji msaidizi.

(2) Taarifa zilizoboreshwa na fomu zilizorejewa chini ya kanuni ndogo ya (1) zitajumuisha-

(a) taarifa za wapiga kura wapya na wapiga kura waliboresha taarifa zao katika mfumo wa kidigitali;

(b) Fomu Na. 1, 3A, 5A na 5B ambazo zimetumika;

(c) kadi za wapiga kura zilizorejeshwa;

(d) Fomu Na. 2 iliyojazwa;

(e) Fomu Na. 1, 3A, 5A na 5B ambazo hazijatumika au zilizoharibika; na

(f) taarifa nyingine yoyote kama ambavyo itaelekezwa na Mkurugenzi wa Uchaguzi.

(3) Endapo afisa mwandikishaji msaidizi atapokea taarifa zilizoboreshwa na fomu kama inavyotakiwa chini ya kanuni ndogo ya (2), atawasilisha au atahakikisha zinawasilishwa kwa afisa mwandikishaji haraka iwezekanavyo.

(4) Afisa mwandikishaji atawasilisha kwa Mkurugenzi wa Uchaguzi taarifa zilizoboreshwa na fomu za kila kituo cha uandikishaji kama zilivyooneshwa katika kanuni ndogo ya (2).

Maandalizi ya Daftari la Awali la Wapiga Kura

**31.** Baada ya kupokea taarifa zilizoboreshwa na fomu kutoka kwenye vituo vya uandikishaji katika kila eneo la uchaguzi, Mkurugenzi wa Uchaguzi ataandaa Daftari la Awali la Wapiga Kura katika kila eneo la uchaguzi kama itakavyoelekezwa na Tume.

Taarifa za Daftari la Awali la Wapiga Kura

**32.-**(1) Daftari la Awali la Wapiga Kura litakuwa na taarifa zifuatazo kwa kila mpiga kura:

(a) jina kama lilivyoandikwa;

(b) jinsi;

(c) tarehe ya kuzaliwa;
(d) namba ya kipekee ya utambuzi wa mpiga kura;
(e) picha;
(f) hali ya ulemavu ikiwa ipo;
(g) kituo cha uandikishaji; na
(h) taarifa nyingine yoyote ambayo Tume itaona ni muhimu.

(2) Daftari la Awali la Wapiga Kura litatumika kwa matumizi yaliyoainishwa katika kifungu cha 11 cha Sheria.

Kuwasilisha Daftari la Awali la Wapiga Kura kwa maafisa waandikishaji

**33**. Baada ya maandalizi ya Daftari la Awali la Wapiga Kura kwa kila eneo la uchaguzi, Mkurugenzi wa Uchaguzi atawapa nakala za Daftari la Awali la Wapiga Kura maafisa waandikishaji kwa idadi ambayo Tume itaamua.

Uwekaji wazi wa Daftari la Awali la Wapiga Kura

**34.** Kwa kuzingatia masharti ya Sheria, Kanuni hizi na maelekezo yatakayotolewa na Tume au Mkurugenzi wa Uchaguzi, afisa mwandikishaji ataweka au kuwezesha kuwekwa wazi kwa Daftari la Awali la Wapiga Kura kwa kila kata kwa ajili ya kukaguliwa na umma katika muda utakaoamuliwa na Tume.

Marekebisho ya taarifa za mpiga kura

**35.-**(1) Mpiga kura ambaye taarifa zake si sahihi katika Daftari la Awali la Wapiga Kura anaweza kuomba kwa mwandishi msaidizi taarifa zake zirekebishwe.

(2) Endapo mwandishi msaidizi ataamua maombi chini ya kanuni hii, atamtaka mwombaji kurejesha kadi ya mpiga kura.

(3) Baada ya mwombaji kurejesha kadi ya mpiga kura kwa mujibu wa kanuni ndogo ya (2), mwandishi msaidizi-

(a) atarekebisha taarifa za mwombaji kwa kujaza Fomu Na. 5A iliyoainishwa kwenye Jedwali la Kwanza; na
(b) atawasilisha kwa afisa mwandikishaji Fomu Na. 5A na Fomu Na. 2 zilizoainishwa kwenye Jedwali la Kwanza pamoja na kadi ya mpiga kura iliyorejeshwa.

Kukosekana kwa jina katika Daftari la Awali la Wapiga Kura

**36.** Endapo jina la mpiga kura aliyeandikishwa halionekani katika Daftari la Awali la Wapiga Kura, mpiga kura huyo anaweza kuomba kwa mwandishi msaidizi taarifa zake ziingizwe katika Daftari la Awali la Wapiga Kura kwa kujaza Fomu Na. 1 iliyoainishwa katika Jedwali la Kwanza na kupewa kadi ya mpiga kura baada ya kurejesha kadi ya awali.

## SEHEMU YA TANO
## PINGAMIZI NA RUFAA

Pingamizi dhidi ya wapiga kura walioandikishwa

**37.-**(1) Mtu hatakuwa na haki ya kupinga kuandikishwa kwa mpiga kura yeyote katika eneo la uchaguzi isipokuwa kama jina lake linaonekana katika Daftari la Awali la Wapiga Kura katika eneo lolote la uchaguzi.

(2) Kwa kuzingatia masharti ya Sheria, pingamizi dhidi ya kuandikishwa au kufutwa kwa jina la mpiga kura yeyote linaweza kuwasilishwa kwa afisa mwandikishaji ndani ya siku saba tangu tarehe ya mwisho ya kuweka wazi Daftari la Awali la Wapiga Kura.

(3) Kila pingamizi litawekwa kwa kujaza nakala mbili za Fomu Na. 3B iliyoainishwa katika Jedwali la Kwanza.

(4) Ndani ya siku saba tangu tarehe ya kupokea pingamizi, afisa mwandikishaji atamjulisha mtu aliyewekewa pingamizi sababu za pingamizi na kumtaka mtu huyo kujibu pingamizi hilo ndani ya siku tatu tangu kupokea taarifa ya pingamizi lililowekwa dhidi yake.

(5) Bila kujali masharti ya kanuni ndogo ya (4), endapo pingamizi limewekwa kwa sababu mtu ambaye jina lake limo katika Daftari la Awali la Wapiga Kura amefariki, afisa mwandikishaji atabandika taarifa ya pingamizi katika mbao za matangazo katika kituo husika.

(6) Kwa kuzingatia kanuni ndogo ya (4), afisa mwandikishaji atapaswa-

(a) kutoa taarifa ya siku saba akiainisha mahali, tarehe na muda wa kufanya uchunguzi wa wazi;

(b) kuendesha uchunguzi wa wazi kuhusiana na

pingamizi; na

(c) kuamua pingamizi na kuwataarifu wahusika kuhusu matokeo.

Rufaa

**38.**-(1) Mtu ambaye hajaridhika na uamuzi wa afisa mwandikishaji, anaweza kukata rufaa Mahakama ya Mwanzo iliyopo katika eneo la uchaguzi ndani ya siku saba tangu uamuzi ulipotolewa.

(2) Mahakama ya Mwanzo itaamua rufaa ndani ya siku kumi na nne tangu tarehe ya kuwasilishwa kwa rufaa na kumpa afisa mwandikishaji maelezo ya uamuzi.

(3) Uamuzi wa Mahakama ya Mwanzo utakuwa wa mwisho.

(4) Kwa kuzingatia masharti ya kanuni ndogo ya (2), afisa mwandikishaji atamjulisha Mkurugenzi wa Uchaguzi kuhusu matokeo ya rufaa na Mkurugenzi wa Uchaguzi ataelekeza kufanyika marekebisho ya Daftari la Awali la Wapiga Kura na kutoa au kufuta kadi ya mpiga kura.

Kuwasilisha taarifa zilizoboreshwa kwa Mkurugenzi wa Uchaguzi

**39.** Baada ya kufanya marekebisho kwenye Daftari la Awali la Wapiga Kura katika eneo la uchaguzi, afisa mwandikishaji atawasilisha kwa Mkurugenzi wa Uchaguzi-

(a) nakala ya uamuzi wa kila pingamizi lililowasilishwa kwa afisa mwandikishaji;

(b) nakala ya maelezo yaliyotolewa na Mahakama ya Mwanzo kuhusu rufaa ya uandikishaji wa mpiga kura yeyote;

(c) taarifa za uandikishaji za wapiga kura zilizojazwa na afisa mwandikishaji pamoja na kadi ya mpiga kura iliyorejeshwa, ikiwa ipo;

(d) nakala ya uamuzi wa maombi ya mapitio uliofanywa na afisa mwandikishaji; na

(e) taarifa nyingine kama itakavyoelekezwa na Tume.

SEHEMU YA SITA

## DAFTARI LA KUDUMU LA WAPIGA KURA NA UTHIBITISHO

Maandalizi ya Daftari

**40.-**(1) Mkurugenzi wa Uchaguzi ataandaa Daftari katika kila eneo la uchaguzi.

(2) Daftari litakuwa na taarifa zifuatazo kwa kila mpiga kura:

(a) jina kama lilivyoandikwa;
(b) jinsi;
(c) tarehe ya kuzaliwa;
(d) namba ya kipekee ya utambuzi wa mpiga kura;
(e) picha;
(f) hali ya ulemavu, ikiwa ipo;
(g) kituo cha uandikishaji; na
(h) taarifa nyingine kama Tume itakavyoamua.

(3) Taarifa zilizoingizwa kwenye Daftari la Awali la Wapiga Kura kwa kila eneo la uchaguzi zitaingizwa kwenye Daftari la eneo hilo la uchaguzi na zitajumuisha-

(a) mtu yeyote aliyeandikishwa katika jimbo au kata;
(b) mtu ambaye jina lake, kwa maoni ya Mkurugenzi wa Uchaguzi, bila kukusudia halikuingizwa kwenye Daftari la Awali la Wapiga Kura la jimbo au kata;
(c) mtu aliyeandikishwa kutokana na uamuzi wa rufaa; na
(d) mtu ambaye maombi yake ya kujumuishwa kwenye Daftari la Awali la Wapiga Kura yamekubaliwa.

(4) Taarifa za mtu yeyote ambaye anaomba kurekebisha au kuhamishwa kwenye Daftari hazitaingizwa iwapo mtu huyo hatajaza Fomu Na. 5A iliyoainishwa kwenye Jedwali la Kwanza.

Uthibitisho wa Daftari

**41.-**(1) Mkurugenzi wa Uchaguzi atalithibitisha Daftari la Kudumu la Wapiga Kura kabla ya kuanza kutumika.

(2) Baada ya uthibitisho wa Daftari chini ya kanuni hii, Daftari lingine lolote la wapiga kura ambalo lilikuwa linatumika katika eneo husika la uchaguzi kabla ya uthibitisho halitatumika.

Kuwasilisha Daftari la Kudumu la Wapiga Kura

**42.** Baada ya kuthibitisha Daftari la Kudumu la Wapiga Kura, Mkurugenzi wa Uchaguzi atawasilisha kwa msimamizi wa uchaguzi nakala za Daftari la Kudumu la Wapiga Kura kwa idadi ambayo Tume itaamua.

Utoaji wa Daftari la Kudumu la Wapiga Kura kwa vyama vya siasa

**43.-**(1) Tume itatoa kwa kila chama cha siasa nakala tepe ya Daftari la Kudumu la Wapiga Kura.

(2) Kwa kuzingatia kanuni ndogo ya (1), chama cha siasa kitatumia nakala tepe ya Daftari kwa madhumuni ya uchaguzi.

Kuingiza, kurekebisha na kubadili taarifa katika Daftari

**44.-**(1) Mkurugenzi wa Uchaguzi anaweza kuingiza, kurekebisha na kufanya mabadiliko kwenye Daftari wakati wowote baada ya kuthibitisha Daftari kwa ajili ya-

(a) kusahihisha makosa yoyote ya kiuandishi;

(b) kurekebisha jina au maelezo yasiyo sahihi; na

(c) kuhakikisha kwamba jina la mtu yeyote halitokei zaidi ya mara moja kwenye Daftari.

(2) Mkurugenzi wa Uchaguzi, kwa madhumuni ya kutekeleza au kuamua jambo lolote chini ya Kanuni hizi, au kujiridhisha kuhusu ulazima wa kufanya marekebisho au mabadiliko yoyote katika Daftari anaweza -

(a) kuamuru mtu yeyote kufika mbele yake kutoa ushahidi;

(b) kusimamia viapo; au

(c) kuamuru kuletwa kwa nyaraka yoyote inayohusika na suala lililo mbele yake.

(3) Endapo Mkurugenzi wa Uchaguzi atafanya masahihisho au mabadiliko kwenye Daftari, atawasilisha nakala ya Daftari lililosahihishwa au kubadilishwa katika eneo la uchaguzi husika.

## SEHEMU YA SABA
## USHIRIKIANO KATIKA MATUMIZI YA VIFAA NA TAARIFA

Makubaliano ya kutumia vifaa na taarifa

**45**.-(1) Kwa kuzingatia masharti ya Kanuni hizi, Tume inaweza kutumia vifaa na taarifa kutoka taasisi nyingine za Serikali kwa madhumuni ya utekelezaji bora

wa zoezi la uboreshaji wa Daftari.

(2) Kwa madhumuni ya kusimamia ushirikiano katika matumizi ya taarifa na vifaa, Tume inaweza kuingia makubaliano na taasisi nyingine za Serikali.

SEHEMU YA NANE
UANGALIZI WA UANDIKISHAJI

Mwaliko na usajili wa waangalizi

**46.-**(1) Kabla ya kuanza mchakato wa uboreshaji wa Daftari, Tume inaweza kutoa mwaliko kwa taasisi, asasi na Serikali kushiriki uangalizi wa uandikishaji.

(2) Mwaliko wa uangalizi wa uandikishaji kwa taasisi na asasi za ndani ya nchi utafanyika kupitia vyombo vya habari vya ndani na mwaliko kwa taasisi, asasi au serikali kutoka nje ya nchi utafanyika kupitia Wizara inayohusika na mambo ya nje.

(3) Taasisi, asasi au serikali inayokusudia kushiriki katika uangalizi wa uandikishaji itaomba kwa Tume kibali cha kuwa mwangalizi wa uandikishaji na kuitaarifu kuhusu nia na mpango wa kutumia timu ya waangalizi wa ndani au wa kimataifa.

(4) Baada ya kupokea maombi, Tume inaweza kukubali au kukataa maombi.

(5) Endapo Tume itakubali maombi, itatoa kitambulisho cha usajili kwa mwangalizi na barua ya utambulisho ambayo atapaswa kuiwasilisha kwa afisa mwandikishaji.

(6) Endapo Tume itakataa maombi, itamtaarifu mwombaji kwa maandishi.

Muda wa uangalizi

**47.-**(1) Uangalizi wa uandikishaji wa Daftari utaanza tarehe ya kusajiliwa hadi tarehe iliyooneshwa katika kitambulisho cha usajili wa mwangalizi.

(2) Tume, kwa uamuzi wake au baada ya kupokea maombi, inaweza kuongeza muda wa uangalizi.

Taarifa na maelezo kwa waangalizi

**48.** Tume inaweza kuwapa waangalizi-

(a) sheria za uchaguzi zinazohusu mchakato wa

uandikishaji na taratibu zinazotumika Tanzania;

(b) mwongozo wa waangalizi wa uandikishaji;

(c) orodha ya mikoa, halmashauri, majimbo, kata na vituo vya uandikishaji;

(d) orodha ya vyama vya siasa vilivyosajiliwa; na

(e) taarifa nyingine muhimu ambazo Tume itaona zinafaa.

Haki na wajibu wa waangalizi

**49.-**(1) Kwa kuzingatia masharti ya Sheria na sheria nyingine yoyote iliyotungwa na Bunge, waangalizi wanaweza kutazama hatua zote za mchakato wa uandikishaji katika vituo vya uandikishaji.

(2) Waangalizi wa uandikishaji hawataruhusiwa kutoa taarifa yoyote kwa umma inayohusu mchakato wa uandikishaji kabla ya kuwasilisha kwa Tume na Tume kukiri kupokea taarifa hiyo.

Kukosa sifa ya kuwa mwangalizi

**50.** Mwangalizi wa uandikishaji atakosa sifa ya uangalizi ikiwa hatazingatia yafuatayo:

(a) miongozo ya waangalizi ambayo imetolewa na Tume;

(b) sheria zinazohusu uandikishaji;

(c) sheria na taratibu za uhamiaji;

(d) sheria yoyote iliyotungwa na Bunge; na

(e) maelekezo mengine yoyote kama yatakavyotolewa na Tume au Mkurugenzi wa Uchaguzi.

Taarifa ya waangalizi wa uandikishaji

**51.-**(1) Kila mwangalizi wa uandikishaji atatoa taarifa kwa Tume au afisa mwandikishaji kuhusu kasoro zinazojitokeza katika mchakato wa uboreshaji wa Daftari.

(2) Kwa kuzingatia masharti ya kanuni hii, baada ya kukamilika kwa kipindi cha uangalizi, kila mwangalizi ataandaa na kuwasilisha taarifa ya uangalizi kwa Tume.

(3) Taarifa ya uangalizi iliyoandaliwa chini ya kanuni ndogo ya (2) itajumuisha yafuatayo:

(a) taarifa za utambulisho za mwangalizi; na

(b) masuala yaliyobainika na mapendekezo.

(4) Taarifa ya uangalizi wa uandikishaji itawasilishwa kwa Tume ndani ya kipindi cha mwezi

mmoja baada kipindi cha uangalizi kukamilika.

## SEHEMU YA TISA
## MAKOSA NA ADHABU

Makosa yanayofanywa na watendaji wa uandikishaji

**52.** Mtendaji wa uandikishaji yeyote ambaye-
(a) kwa udanganyifu anahamisha au anasababisha kuhamisha taarifa yoyote ya uandikishaji; au
(b) anatoa kwa mtu kadi ya mpiga kura kinyume na ilivyoelekezwa na Kanuni hizi,

anatenda kosa.

Kughushi, kufuta, au kuharibu taarifa

**53.** Mtu yeyote ambaye anaghushi, anafuta au kwa nia ovu anaharibu taarifa za kuandikishwa anatenda kosa.

Kumiliki nyaraka za kughushi

**54.** Mtu yeyote anayemiliki nyaraka za uandikishaji au kadi ya mpiga kura iliyoghushiwa anatenda kosa.

Taarifa za uongo

**55.** Mwombaji, mweka pingamizi au mrufani ambaye kwa makusudi anajaza taarifa za uongo katika fomu ya maombi, pingamizi, rufaa au tamko, anatenda kosa.

Kukaidi kuondoka katika eneo la uandikishaji

**56.** Mtu yeyote ambaye anakataa kuondoka katika eneo lolote linalotumiwa kwa ajili ya shughuli za uandikishaji wa wapiga kura au masuala yaliyoainishwa katika Kanuni hizi, baada ya mtendaji wa uandikishaji kumtaka kuondoka katika eneo hilo, anatenda kosa.

Uchapishaji na uharibifu wa zana usioruhusiwa

**57.** Mtu yeyote ambaye-
(a) bila kuwa na mamlaka halali anaharibu zana za uandikishaji zilizobandikwa; au
(b) anachapa au kusambaza zana yoyote ya uandikishaji bila idhini ya Tume au afisa mwandikishaji,

anatenda kosa.

Adhabu

**58.** Mtu yeyote ambaye anatenda kosa chini ya Kanuni hizi, akitiwa hatiani atawajibika kulipa faini

isiyopungua shilingi laki moja na isiyozidi shilingi laki tatu au kutumikia kifungo kwa kipindi kisichopungua miezi sita na kisichozidi miaka miwili au vyote kwa pamoja.

SEHEMU YA KUMI
MASHARTI MENGINEYO

Kurejesha kadi ya mpiga kura aliyefariki

**59.-**(1) Endapo mpiga kura amefariki, mpiga kura mwenye kadi ya mpiga kura aliyefariki atapaswa kuirudisha kadi hiyo kwa afisa mwandikishaji mapema iwezekanavyo wakati wa uboreshaji wa Daftari.

(2) Afisa mwandikishaji atamtaka mpiga kura aliyerejesha kadi ya mpiga kura aliyefariki kujaza Fomu Na. 5B. iliyoainishwa kwenye Jedwali la Kwanza.

(3) Afisa mwandikishaji atawasilisha kwa Mkurugenzi wa Uchaguzi Fomu Na. 5B pamoja na kadi ya mpiga kura iliyorejeshwa.

Uchapishaji wa notisi

**60.** Endapo notisi inapaswa kutangazwa kwa mujibu wa Kanuni hizi, na kwa maoni ya Tume, namna ya utangazaji iliyoainishwa haifikishi taarifa ipasavyo, pamoja na kuitangaza notisi hiyo kwa mujibu wa Kanuni hizi, Tume inaweza kubandika nakala za notisi hiyo katika eneo maarufu ndani ya eneo ambalo notisi inahusika au kuchukua hatua nyingine muhimu ili kuhakikisha notisi hiyo inatangazwa ipasavyo.

Kufutwa kwa Kanuni
TS. Na.
793 la 2018
792 la 2018

**61.** Kanuni za Uchaguzi wa Rais na Wabunge (Uboreshaji wa Daftari la Kudumu la Wapiga Kura) za Mwaka 2018 na Kanuni za Uchaguzi wa Serikali za Mitaa (Uboreshaji wa Daftari la Kudumu la Wapiga Kura) za Mwaka 2018 zinafutwa.

*Tangazo la Serikali Na. 389 (Linaendelea.)*

JEDWALI LA KWANZA

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
TUME HURU YA TAIFA YA UCHAGUZI
(UANDIKISHAJI KWA AJILI YA UCHAGUZI WA RAIS, WABUNGE NA MADIWANI)

FOMU NA. 1

OMBI LA KUANDIKISHWA KUWA MPIGA KURA

*(imetengenezwa chini ya kanuni ya 21(2) na 36)*

(FOMU HII IJAZWE KWA HERUFI KUBWA KWA KALAMU YA WINO MWEUSI AU BULUU)

INEC 000000001

A: TAARIFA BINAFSI ZA MWOMBAJI
*Personal Particulars*

1. JINA LA KWANZA *First Name*
2. JINA LA KATI *Middle Name*
3. JINA LA MWISHO *Last Name*
4. JINSI *Sex* (a) ME *Male* (b) KE *Female*
5. NAMBA YA NIDA. (Kama ipo) *NIN*
6. (a) TAREHE YA KUZALIWA *Date of Birth* D D M M Y Y Y Y
   (b) Kama mwombaji ni MTU MZIMA na hakumbuki tarehe au mwaka wa kuzaliwa (weka alama ya √ hapa) *If the applicant is an ADULT and does not remember his/her date of birth tick √ here*
7. (a) MKOA ALIPOZALIWA *Region of birth*
   (b) HALMASHAURI YA JIJI/MANISPAA/MJI/WILAYA * *City/Municipal/Town/District Council of birth*
8. URAIA *Citizenship*
   (a) Kwa kuzaliwa *By Birth* — Mahali pa Kuzaliwa *Place of Birth* (i) Nchini *Tanzania* (ii) Nje ya nchi *Foreign Country*
   (b) Kwa kuandikishwa *By registration* — (i) Tarehe ya kuandikishwa *Date of registration of citizenship* D D M M Y Y Y Y — (ii) Mahali pa kuandikishwa (Mkoa) *Place of Registration(Region)*
   (iii) Namba ya Hati ya Tajinisi *Number of certificate of registration/ Naturalization Number*
9. KAZI *Occupation*

B: ANUANI YA MWOMBAJI / MAKAZI YA MWOMBAJI KWA SASA
*Current Applicant's Address / Residence*

10. NAMBA YA NYUMBA *House Number*
11. KATA / SHEHIA * *Ward / Shehia*
12. MTAA / KIJIJI * *Street / Village*
13. KITONGOJI
14. ANUANI YA POSTA *Address*
15. POSTKODI *Postcode*
16. NAMBA YA SIMU *Telephone Number*

C: ANUANI YA KUDUMU / MAKAZI YA KUDUMU YA MWOMBAJI
*Permanent Applicant's Address / Residence*

17. MKOA *Region*
18. HALMASHAURI YA JIJI / MANISPAA / MJI / WILAYA* *City/Municipal/Town/District Council*
19. KATA / SHEHIA * *Ward / Shehia*
20. MTAA / KIJIJI * *Street / Village*
21. KITONGOJI

D: TAARIFA ZA ULEMAVU
*Disability Informatiom*

22. HALI YA ULEMAVU *Disability status*

E: TAMKO NA SAINI YA MWOMBAJI
*Applicant's Declaration and Signature*

23. Mimi.................................................................................................. ....................................................niliyetoa taarifa zangu kuwa Mpiga Kura katika Kituo/Kijiji/Mtaa/ Kitongoji/ Kata / Shehia iliyotajwa hapo juu natoa tamko kuwa maelezo niliyoyatoa ni sahihi. *
*I..............................................who stated my particulars to be a Voter in Registration Centre/Street/Village or Ward/Shehia stated above, I do hereby confirm that the particulars stated above are correct.*
24. SAINI YA MWOMBAJI *Applicant's Signature*
25. KWA MWOMBAJI ASIYEWEZA KUSAINI, SABABU YA KUTOWEKA SAINI *For Applicant who is not able to sign, reason for not signing* — (a) Mwombaji hawezi kuandika *Applicant unable to write* — (b) Mwombaji ni Mlemavu wa mikono *Applicant has hand disability*

F: TAARIFA ZA MWANDISHI MSAIDIZI
*Particulars of Registration Assistant*

26. JINA KAMILI LA MWANDISHI MSAIDIZI *Full name of registration assistant*
27. NAMBA YA SIMU *Telephone Number*
30. TAREHE YA KUANDIKISHA *Date of Registration* D D M M Y Y Y Y
31. JINA LA KITUO *Name of Registration Centre*
32. NAMBA YA KITUO *Registration Centre number*
33. SAINI *Signature*

**Futa isiyotakiwa/Delete whichever is unapplicable*

*Tangazo la Serikali Na. 389 (Linaendelea.)*

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

# TUME HURU YA TAIFA YA UCHAGUZI

FOMU NA.

**(UANDIKISHAJI KWA AJILI YA UCHAGUZI WA RAIS, WABUNGE NA MADIWANI)**

# 2

## MAJUMUISHO YA IDADI YA FOMU NA KADI KWA SIKU

*(Imetengenezwa chini ya kanuni ya 21(5), 24(5), 25(3), 26(2) (c) na 28(6))*

| JINA LA KITUO | KATA | HALMASHAURI |
|---|---|---|
| | | |

| **Idadi ya fomu na kadi zilizotolewa** | | | | | | **Idadi ya fomu na kadi zilizoharibika** | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| siku | Fomu Na. 1 | Fomu Na. 5A | Fomu Na. 5B | Kadi | | Fomu Na. 1 | Fomu Na. 5A | Fomu Na. 5B | Kadi |
| Siku 1 | | | | | | | | | |
| Siku 2 | | | | | | | | | |
| Siku 3 | | | | | | | | | |
| Siku 4 | | | | | | | | | |
| Siku 5 | | | | | | | | | |
| Siku 6 | | | | | | | | | |
| Siku 7 | | | | | | | | | |
| Siku 8 | | | | | | | | | |
| Siku 9 | | | | | | | | | |
| Siku 10 | | | | | | | | | |
| Siku 11 | | | | | | | | | |
| Siku 12 | | | | | | | | | |
| Siku 13 | | | | | | | | | |
| Siku 14 | | | | | | | | | |
| Siku 15 | | | | | | | | | |
| Siku 16 | | | | | | | | | |
| Siku 17 | | | | | | | | | |
| Siku 18 | | | | | | | | | |
| Siku 19 | | | | | | | | | |
| Siku 20 | | | | | | | | | |
| **JUMLA** | | | | | | | | | |

| Jina kamili la Mwandishi | Saini | Tarehe |
|---|---|---|
| | | |

OFISI YA MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI TANZANIA
WELEDI NA UBORA
PROFESSIONALISM & EXCELLENCE
THE OFFICE OF THE ATTORNEY GENERAL TANZANIA

*Tangazo la Serikali Na. 389 (Linaendelea.)*

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**TUME HURU YA TAIFA YA UCHAGUZI**
(UANDIKISHAJI KWA AJILI YA UCHAGUZI WA RAIS, WABUNGE NA MADIWANI)

UAMUZI WA KUTOKUBALI OMBI LA KUANDIKISHWA KUWA MPIGA KURA

*(Imetengenezwa chini ya kanuni ya 23(2))*

**FOMU NA.**

# 3A

Halmashauri/Wilaya: ..........................................................................................................
Jimbo la Uchaguzi:...............................................................................................................
Kata/Shehia:......................................................................................................................
Kituo cha kuandikisha wapiga kura:.....................................................................................
Tarehe: ……………………………………………........…………………………………
Jina kamili la aliyeomba kuandikishwa:...............................................................................
Anuani ya makazi kama ilivyotolewa na mwombaji:...........................................................
Jinsi (me/ke):......................................................................................................................
Umri kama alivyotaja mwombaji:.........................................................................................
Saini ya aliyeomba kuandikishwa:.....................................................................................

**UTHIBITISHO WA MWANDISHI MSAIDIZI**

Nathibitisha kwamba nimekataa kumwandikisha mwombaji ambaye taarifa zake zimetajwa hapo juu kwa sababu zifuatazo:

| Na. | Sababu | Weka alama (V) panapohitajika | Saini ya Mwandishi Msaidizi |
|---|---|---|---|
| 1. | Si raia wa Tanzania | | |
| 2. | Si mkazi wa kawaida katika jimbo au kata ambayo anaomba kuandikishwa | | |
| 3. | Hajatimiza umri wa miaka 18 na hatatimiza umri huo ifikapo siku ya uchaguzi | | |
| 4. | Ana utii wa nchi nyingine tofauti na Tanzania | | |
| 5. | Amethibitika kisheria kwamba hana akili timamu | | |
| 6. | Amewekwa kizuizini kwa Amri ya Rais | | |
| 7. | Kwa mujibu wa Sheria za Uchaguzi au Sheria nyingine zinazotumika Tanzania amepoteza sifa kuwa mpiga kura kutokana na makosa yanayoambatana na uchaguzi. | | |
| 8. | Amehukumiwa kifo au kifungo cha zaidi ya miezi sita | | |

Jina kamili la mwandishi msaidizi:.......................................................................................
Saini yake:..........................................................................................................................
Jina kamili la aliyekataliwa:..................................................................................................
Maoni ya aliyekataliwa kuandikishwa: ……………………………………………………
**MAELEZO YA ALIYEKATALIWA**

*Tangazo la Serikali Na. 389 (Linaendelea.)*

*Naridhika/siridhiki na uamuzi wa mwandishi msaidizi kwa sababu zifuatazo:
...................................................................................................................................
Saini ya aliyekataliwa: …………………………………………………………………..
Tarehe: ……………………………………………………………………………...

**UTHIBITISHO WA MAWAKALA WA UANDIKISHAJI, IKIWAWAPO**

Tunathibitisha hivi ndivyo ilivyokuwa kwenye kituo cha kuandikisha wapiga kura (Sehemu hii ijazwe na mawakala wa uandikishaji)

| Na. | Jina | Chama | Saini |
|---|---|---|---|
| 1. | ……………………….…… | ……………………… | …………………….. |
| 2. | ……………………….…… | …………………… | …………………….. |
| 3. | ……………………….…… | ……………………… | …………………….. |
| 4. | ……………………….…… | ……………………… | …………………….. |
| 5. | ……………………….…… | …………………… | ……………………. |
| 6. | ……………………….…… | …………………… | …………………….. |
| 7. | ……………………….…… | ……………………… | …………………….. |
| 8. | ……………………….…… | ……………………… | …………………….. |
| 9. | ……………………….…… | ……………………… | …………………….. |
| 10. | ……………………….…… | ……………………… | …………………….. |
| 11. | ……………………….…… | …………………… | …………………….. |
| 12. | ……………………….…… | …………………… | …………………….. |
| 13. | ……………………….…… | ……………………… | …………………….. |
| 14. | ……………………….…… | ……………………… | …………………….. |
| 15. | ……………………….…… | ……………………… | …………………….. |
| 16. | ……………………….…… | ……………………… | …………………….. |
| 17. | ……………………….…… | ……………………… | …………………….. |
| 18. | ……………………….…… | ……………………… | …………………….. |
| 19. | ……………………….…… | …………………… | …………………….. |
| 20. | ……………………….…… | ……………………… | …………………….. |

Uamuzi wa Afisa mwandikishaji na sababu za uamuzi huo
…..........…………………………………………………………………………………..
Jina kamili la Afisa mwandikishaji:.............................................................................................
Saini ya Afisa mwandikishaji:......................................................................................................
Tarehe: ……………………………………………………………………………...

*Futa isiyotakiwa

OFISI YA MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI TANZANIA · WELEDI NA UBORA · PROFESSIONALISM & EXCELLENCE · THE OFFICE OF THE ATTORNEY GENERAL TANZANIA

*Tangazo la Serikali Na. 389 (Linaendelea.)*

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**TUME HURU YA TAIFA YA UCHAGUZI**

(UANDIKISHAJI KWA AJILI YA UCHAGUZI WA RAIS, WABUNGE NA MADIWANI)

FOMU NA.

# 3B

KUPINGA KUENDELEA KUWEPO KWA JINA LOLOTE KATIKA DAFTARI LA KUDUMU LA WAPIGA KURA

*(Imetengenezwa chini ya kanuni ya 37(3))*

Halmashauri/Wilaya:.........................................................................................................
.

Jimbo la Uchaguzi:.........................................................................................................

Kata/Shehia:.........................................................................................................

SEHEMU YA KWANZA

**TAARIFA ZA ANAYEOMBA JINA LAKE AU LA MTU MWINGINE LIFUTWE KATIKA DAFTARI LA KUDUMU LA WAPIGA KURA**

1. Jina Kamili:…………………………………………………………………….
2. Jina la Kituo ambacho alijiandikisha:.........................................................................
3. Tarehe aliyojiandikisha:……………………………………………………….
4. Namba ya kadi ya mpiga kura:.....................................................................................
5. Anuani ya posta au makazi: .........................................................................................
   .........................................................................................................
   .........................................................................................................
   .........................................................................................................

OFISI YA MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI TANZANIA
THE OFFICE OF THE ATTORNEY GENERAL TANZANIA
PROFESSIONALISM & EXCELLENCE

*Tangazo la Serikali Na. 389 (Linaendelea.)*

SEHEMU YA PILI

**TAARIFA ZA MTU AMBAYE JINA LAKE LINAOMBWA LIFUTWE KATIKA DAFTARI LA KUDUMU LA WAPIGA KURA**

1. Jina kamili (kama ilivyoandikwa katika Daftari la Kudumu la Wapiga Kura): ..........................................................................................................................
2. Jina la kituo alichoandikishwa:.................................................................................
3. Namba ya Kadi ya Mpiga Kura: ................................................................................

***Angalizo:*** Kama jina linaloombwa kuondolewa ni la muombaji mwenyewe atajaza kama sehemu ya kwanza.

SEHEMU YA TATU

**SABABU ZA KUTAKA JINA LA MTU KUFUTWA KATIKA DAFTARI LA KUDUMU LA WAPIGA KURA**

*Wakati wa kuandikishwa sikuwa/hakuwa na sifa zinazohitajika kuwa Mpiga Kura.
*Wakati wa kuandikishwa nilikuwa nina sifa/alikuwa ana sifa zinazohitajika kuwa Mpiga Kura lakini sasa sistahili/hastahili tena kuwa Mpiga Kura.

| Na. | Sababu | Weka alama (V) panapohitajika | Saini ya anayepinga |
|---|---|---|---|
| 1. | Si raia wa Tanzania | | |
| 2. | Si mkazi wa kawaida katika jimbo au kata ambayo anaomba kuandikishwa | | |
| 3. | Hajatimiza umri wa miaka 18 na hatakuwa ametimiza umri huo ifikapo siku ya uchaguzi | | |
| 4. | Ana utii wa nchi nyingine zaidi ya Tanzania | | |
| 5. | Amethibitika kisheria kwamba hana akili timamu | | |
| 6. | Amewekwa kizuizini kwa Amri ya Rais | | |
| 7. | Kwa mujibu wa Sheria za Uchaguzi au Sheria nyingine zinazotumika Tanzania amepoteza sifa kuwa mpiga kura kutokana na makosa yanayoambatana na uchaguzi | | |
| 8. | Amehukumiwa kifo/kifungo zaidi ya miezi sita | | |

***Futa isiyohitajika.**

SEHEMU YA NNE

**KUMBUKUMBU YA AFISA MWANDIKISHAJI**

1. Tarehe ya uchunguzi wa wazi wa pingamizi: …………………………………
2. Majina ya walioitwa katika uchunguzi.
   ........................................................................................................................
   ........................................................................................................................
   ........................................................................................................................
   ........................................................................................................................

3. Jina kamili la aliyechunguza na kufanya uamuzi.
............. ........................................................................................................................

4. Uamuzi uliotolewa.
............. .................................……………………………………………………………
............. .................................……………………………………………………………

Saini:…………………………………………………………
Wadhifa: Afisa mwandikishaji/Afisa mwandikishaji msaidizi
Tarehe:………………………………………………………

*Tangazo la Serikali Na. 389 (Linaendelea.)*

**JAMHURI YA MUUNGANO WATANZANIA**

**TUME HURU YA TAIFA YA UCHAGUZI**

(UANDIKISHAJI KWA AJILI YA UCHAGUZI WA RAIS, WABUNGE NA MADIWANI)

**FOMU NA.**

**4**

**MKATABA WA AJIRA YA MUDA**

*(Imetengenezwa chini ya kanuni ya 11(5) na 12(1)(f))*

Mkataba huu umefanyika leo tarehe …………Mwezi…….…………. Mwaka ………..

**KATI YA**

**AFISA MWANDIKISHAJI** wa Jimbo la ............................................................................ (ambaye kwa madhumuni ya mkataba huu atajulikana kama "MWAJIRI") kwa upande mmoja;

**NA**

Ndugu ………………………... ……………. wa S. L. P. ................................................. (ambaye kwa madhumuni ya mkataba huu atajulikana kama "MWAJIRIWA") kwa upande wa pili;

**KWA KUWA** Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi imepewa jukumu la Kikatiba la kusimamia na kuratibu uandikishaji wa wapiga kura; na

**KWA KUWA** Afisa Mwandikishaji amepewa jukumu la kuajiri mwandishi msaidizi na mwendesha kifaa cha kibayometriki wa uandikishaji wapiga kura katika jimbo analoliongoza;

**HIVYO, MKATABA HUU UNASHUHUDIA MAKUBALINO YAFUATAYO:**

1. Kwamba, mwajiri amekubali kumuajiri mwajiriwa na mwajiriwa amekubali kuajiriwa katika nafasi ya ………………………. kuanzia tarehe …. mwezi ………mwaka …… hadi tarehe …... mwezi ……… mwaka…………… kwa malipo ya shilingi ………………………... kwa siku.
2. Kwamba, malipo yatafanyika kwa awamu mbili kama ifuatavyo-
   (a) Mwajiriwa atalipwa malipo ya awali tarehe ya kuanza kazi.
   (b) Mwajiriwa atalipwa kiasi cha malipo kilichobaki siku ya kukabidhi vifaa baada ya kumaliza zoezi la uandikishaji.
3. Kwamba, mwajiri hatamlipa mwajiriwa malipo kwa siku ambazo atashindwa kufika kwenye kituo cha kazi kutekeleza majukumu yake.
4. Kwamba, mwajiri ataandaa mafunzo ya namna mwajiriwa atakavyotekeleza majukumu yake.
5. Kwamba, katika mafunzo hayo mwajiri atamlipa mwajiriwa shilingi.………..……… kwa kila siku atakayohudhuria mafunzo nje ya malipo ya siku za mkataba.
6. Kwamba, mwajiri anaweza kusitisha mkataba ikiwa mwajiriwa atakiuka masharti ya mkataba wa ajira.
7. Kwamba, mwajiri au mwakilishi wake anayo haki ya kukagua vifaa vya uandikishaji kila atakapoona inafaa kufanya hivyo kipindi chote cha mkataba.

*Tangazo la Serikali Na. 389 (Linaendelea.)*

8. Kwamba, mwajiriwa atawajibika kuandikisha wapiga kura, kusimamia na kuratibu shughuli za uboreshaji wa Daftari la Kudumu la Wapiga Kura katika kituo cha uandikishaji.
9. Kwamba, mwajiriwa atawajibika kutunza vifaa vyote alivyokabidhiwa katika hali ya usalama kwa muda wote wa ajira na kuvikabidhi kwa mwajiri siku ya mwisho ya mkataba.
10. Kwamba mwajiriwa akiharibu kwa makusudi au kwa uzembe vifaa vya uandikishaji atawajibika kufidia hasara aliyoisababisha.
11. Kwamba, katika utekelezaji wa majukumu yake mwajiriwa anapaswa kuonesha nidhamu na uadilifu kwa mwajiri wake muda wote.
12. Kwamba, mwajiriwa hataruhusiwa kufanya mgomo katika kipindi chote cha ajira na ikiwa atafanya hivyo atawajibika kufidia hasara yoyote atakayokuwa amesababisha.
13. Kwamba, mwajiriwa anaweza kusitisha mkataba kwa kutoa Notisi ya saa 48 ikiwa masharti ya mkataba yatakiukwa.
14. Kwamba, Mwajiri anaweza kuongeza muda wa mkataba kadri atakavyoona inafaa.

Mkataba huu umesainiwa na pande husika leo tarehe …………Mwezi ………
Mwaka…......

**Jina la mwajiri..............................................................**
**Cheo: ..........................................................................**
**Saini... .........................................................................**
**Muhuri:.......................................................................**
**.......................................................................................**
**Jina la mwajiriwa: ..........................................................**
**Cheo: ...........................................................................**
**Saini:..............................................................................**

OFISI YA MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI TANZANIA
WELEDI NA UBORA
PROFESSIONALISM & EXCELLENCE
THE OFFICE OF THE ATTORNEY GENERAL TANZANIA

*Tangazo la Serikali Na. 389 (Linaendelea.)*

FOMU NA.
**5A**

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
TUME HURU YA TAIFA YA UCHAGUZI
(UANDIKISHAJI KWA AJILI YA UCHAGUZI WA RAIS, WABUNGE NA MADIWANI)

OMBI LA KUHAMISHA / KUSAHIHISHA TAARIFA ZA MPIGA KURA / KUPATIWA KADI MPYA

*(imetengenezwa chini ya kanuni ya 24(2)(b), 24(4) na 35(3)(a))*

(FOMU HII IJAZWE KWA HERUFI KUBWA KWA KALAMU YA WINO MWEUSI AU BULUU)

INEC 000000001

A: TAARIFA BINAFSI ZA MWOMBAJI
*Personal Particulars*

1. JINA LA KWANZA *First Name*
2. JINA LA KATI *Middle Name*
3. JINA LA MWISHO *Last Name*
4. JINSI *Sex* (a) ME *Male* (b) KE *Female*
5. NIDA NA. (Kama ipo) *NIN*
6. (a) TAREHE YA KUZALIWA *Date of Birth* D D M M Y Y Y Y
(b) Kama mwombaji ni MTU MZIMA na hakumbuki tarehe au mwaka wa kuzaliwa (weka alama ya √ hapa) *If the applicant is an ADULT and does not remember his/her date of birth tick √ here*
7. (a) MKOA ALIPOZALIWA *Region of birth*
(b) HALMASHAURI YA JIJI/MANISPAA/MJI/WILAYA * *City/Municipal/Town/District Council of birth*
8. URAIA *Citizenship* (a. Kwa kuzaliwa *By Birth* i. Mahali pa Kuzaliwa *Place of Birth* a. Nchini *Tanzania* b. Nje ya nchi *Foreign Country*
(b) Kwa kuandikishwa i. Tarehe ya kuandikishwa *Date of registration of citizenship* D D M M Y Y Y Y ii. Mahali pa kuandikishwa (Mkoa) *Place of Registration(Region)*
iii. Namba ya Hati ya Tajinisi *Number of certificate of registration/ Naturalization Number*
9. KAZI *Occupation*

B: ANUANI YA MWOMBAJI / MAKAZI YA MWOMBAJI KWA SASA
*Current Applicant's Address / Residence*

10. NAMBA YA NYUMBA *House Number*
11. KATA / SHEHIA * *Ward / Shehia*
12. MTAA / KIJIJI * *Street / Village*
13. KITONGOJI
14. ANUANI YA POSTA *Address*
15. POSTKODI *Postcode*
16. NAMBA YA SIMU *Telephone Number*

C: KUMBUKUMBU BINAFSI
*Personal Records*

17. NAMBA YA KADI YA AWALI (Kama ipo) *Number of Previous Card (If available)*
18. KITUO CHA MWISHO ALICHOJIANDIKISHA MPIGA KURA *The last Registration Centre*
19. MTAA / KIJIJI / KITONGOJI * *Street / Village / Kitongoji*
20. KATA / SHEHIA * *Ward / Shehia*

D: SABABU ZA MAREKEBISHO
*Reasons for Amendment*

21. MATUMIZI YA FOMU *Use of form* (a) MASAHIHISHO *Corrections* (b) KADI IMEHARIBIKA / IMEPOTEA *Defaced / Lost card* (c) UHAMISHO *Transfer* (Weka alama ya √ ) *Tick √*

E: TAARIFA ZA ULEMAVU NA SAINI YA MWOMBAJI
*Disability Information and Applicant's Signature*

22. HALI YA ULEMAVU *Disability status*
23. SAINI YA MWOMBAJI *Applicant's Signature*
24. KWA MWOMBAJI ASIYEWEZA KUSAINI, SABABU YA KUTOWEKA SAINI *For Applicant who is not able to sign, reason for not signing* (a).Mwombaji hawezi kuandika *Applicant unable to write* (b) Mwombaji ni Mlemavu *Applicant has disability*

F: TAMKO LA MWOMBAJI IKIWA KADI IMEHARIBIKA/IMEPOTEA/IMEFUTIKA
*Applicant's Declaration*

25. Mimi.................................................. ..................................niliyeandikishwa kuwa Mpiga Kura katika Kituo/Kijiji/Mtaa/Kitongoji/Kata/Shehia iliyotajwa hapo juu natoa tamko kuwa Kadi yangu imeharibika/imepotea / imefutika. *
*I........................................................ who was registered as a Voter in Registration Centre/Village or Ward/Shehia stated above, I do hereby confirm that the particulars states above are correct.*
26. SAINI YA MWOMBAJI *Applicant's Signature*

G: TAARIFA ZA MWANDISHI MSAIDIZI
*Particulars of Registration Assistant*

27. JINA KAMILI LA MWANDISHI MSAIDIZI *Full name of Registration Assistant*
28. NAMBA YA SIMU *Telephone Number*
30. TAREHE YA KUANDIKISHA *Date of Registration* D D M M Y Y Y Y
31. JINA LA KITUO *Name of Registration Centre*
32. NAMBA YA KITUO *Registration Centre number*
33. SAINI *Signature*

**Futa isiyotakiwa/Delete whichever is unapplicable*

*Tangazo la Serikali Na. 389 (Linaendelea.)*

FOMU NA.
**5B**

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
TUME HURU YA TAIFA YA UCHAGUZI

(UANDIKISHAJI KWA AJILI YA UCHAGUZI WA RAIS, WABUNGE NA MADIWANI)

OMBI LA KUFUTA TAARIFA ZA MPIGA KURA

*(imetengenezwa chini ya kanuni ya 28)*

(FOMU HII IJAZWE KWA HERUFI KUBWA KWA KALAMU YA WINO MWEUSI AU BULUU)

INEC 000000001

A: TAARIFA ZA MPIGA KURA ANAYETAKIWA KUFUTWA KWENYE DAFTARI
*Particulars of a Voter who is to be deleted from the Register*

1. NAMBA YA KADI YA MPIGA KURA *Voter's Identification Number*
2. JINA LA KWANZA *First Name*
3. JINA LA KATI *Middle Name*
4. JINA LA MWISHO *Last Name*
5. TAREHE YA KUZALIWA *Date of birth* D D M M Y Y Y Y
6. KITUO ALICHOJIANDIKISHA MPIGA KURA *Registration Centre of a Voter whose name is to be deleted*
   (a) Mkoa *Region*
   (b) Halmashauri/Wilaya * *Council*
   (c) Kata / Shehia *Ward/Shehia*
   (d) Jina la Kituo *Name of Registration Centre*
7. KADI YA MPIGA KURA IMEREJESHWA *Voter's Card has been surrendered* (a) Ndio *Yes* (b) Hapana *No* (Weka alama ya √) *Tick √*
8. SABABU YA KUFUTWA (Tazama geresho lililopo ukurasa namba 2) *Reason for deletion (see the code on the page number 2.)*

B: TAARIFA ZA MTOA TAARIFA
*Particulars of the reporting person*

9. JINA LA KWANZA *First Name*
10. JINA LA KATI *Middle Name*
11. JINA LA MWISHO *Last Name*
12. NAMBA YA KADI YA MPIGA KURA *Voter's Identification Number*
13. TAREHE YA KUZALIWA *Date of birth* D D M M Y Y Y Y
14. ENEO ANALOISHI MPIGA KURA *Residential area of a person reporting a Voter whose particulars is to be deleted*
   (a) KATA / SHEHIA * *Ward / Shehia*
   (b) MTAA / KIJIJI * *Street / Village*
   (c) NAMBA YA SIMU *Telephone number*

C: TAMKO LA MTOA TAARIFA
*Declaration of the reporting person*

15. MIMI *I* ______ Niliyeandikishwa kuwa Mpiga Kura katika: *Registered as a Voter in*
   (a) Kituo *Registration Centre*
   (b) Kata / Shehia * *Ward / Shehia*
   (c) Halmashauri *Council*
   Natoa tamko kuwa maelezo niliyoyatoa ni sahihi. *I hereby declare that the statement stated above are correct.*
16. SAINI YA ALIYETOA TAARIFA *Signature of a reporting person*
17. Tarehe *Date* D D M M Y Y Y Y

D: TAARIFA ZA MWANDISHI MSAIDIZI
*Particulars of Registration Assistant*

18. JINA KAMILI LA MWANDISHI MSAIDIZI *Full name of Registration Assistant*
19. NAMBA YA SIMU *Telephone Number*
20. TAREHE YA KUANDIKISHA *Date of Registration* D D M M Y Y Y Y
21. JINA LA KITUO *Full name of Registration Centre*
22. NAMBA YA KITUO *Registration Centre number*
23. SAINI *Signature*

**Futa isiyotakiwa/Delete whichever is unapplicable*

1

*Tangazo la Serikali Na. 389 (Linaendelea.)*

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**TUME HURU YA TAIFA YA UCHAGUZI**

(UANDIKISHAJI KWA AJILI YA UCHAGUZI WA RAIS, WABUNGE NA MADIWANI)

FOMU NA.

**6**

**KIAPO CHA KUJITOA UANACHAMA AU KUTOKUWA MWANACHAMA WA CHAMA CHA SIASA**

*(Imetengenezwa chini ya kanuni ya 10(a) na 12(3)(a ))*

Mimi .......................................................................................................................................

Niliyeteuliwa/niliyeajiriwa kuwa..............................................................................................
Naapa/Nathibitisha kwamba: -

1. Mimi si mwanachama wa chama cha siasa ☐

AU

2. Mimi ni mwanachama wa chama cha siasa ☐
…………………………………………………….

Najitoa katika chama hicho cha siasa kuanzia leo tarehe……… Mwezi wa ……..…….. Mwaka …………

Naapa/Nathibitisha nikiamini kwamba kiapo hiki ni cha kweli.

Jina......................................................... Wadhifa: …………………………………………

Leo tarehe …………. Mwezi wa …………… Mwaka ...............

.....................................
Saini ya mtoa kiapo.

Kiapo hiki kimetolewa mbele ya (Jina) ....................................................................................

…………………….....................
(Saini na Muhuri wa)
*Hakimu/ Afisa mwandikishaji

***Futa isiyohitajika**

Weka ya vema (√) katika kisanduku husika

OFISI YA MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI TANZANIA
WELEDI NA UBORA
PROFESSIONALISM & EXCELLENCE
THE OFFICE OF THE ATTORNEY GENERAL TANZANIA

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**TUME HURU YA TAIFA YA UCHAGUZI**

(UANDIKISHAJI KWA AJILI YA UCHAGUZI WA RAIS, WABUNGE NA MADIWANI)

FOMU NA.

**7**

**KIAPO CHA KUTUNZA SIRI**

*(Imetengenezwa chini ya kanuni ya 10(b) na 12(3)(b))*

Mimi ……………………………………………………………………………

Niliyeteuliwa/niliyeajiriwa kuwa……………………………………………..

*Naapa / Nathibitisha kwamba sitatoa siri kwa mtu yeyote kuhusu jambo lolote nitakalolijua au nitakaloliona kutokana na kuteuliwa/kuajiriwa kwangu, ila kama nitaruhusiwa kufanya hivyo kwa mujibu wa Sheria.

……………………………

Saini

*Ameapa/Amethibitisha mbele yangu leo tarehe ……Mwezi…..….Mwaka………….

Jina......................................................................................

Saini....................................................................................

…………………………………………………………..

* Muhuri wa Hakimu/Afisa mwandikishaji

***Futa isiyohitajika**

OFISI YA MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI TANZANIA
WELEDI NA UBORA
PROFESSIONALISM & EXCELLENCE
THE OFFICE OF THE ATTORNEY GENERAL TANZANIA

*Tangazo la Serikali Na. 389 (Linaendelea.)*

## JEDWALI LA PILI

*(Limetengenezwa chini ya kanuni ya 16(2))*

### UTARATIBU UTAKAOTUMIKA KUANDIKISHA WAFUNGWA AU WANAFUNZI WA VYUO VYA MAFUNZO NA MAHABUSU KATIKA DAFTARI LA KUDUMU LA WAPIGA KURA

1. Kituo cha kuandikisha wapiga kura gerezani au chuo cha mafunzo
   (i) Kwa madhumuni ya kuandikisha wapiga kura au kuboresha taarifa za wapiga kura ambao ni wafungwa waliopo gerezani au wanafunzi wa vyuo vya mafunzo, Tume itaanzisha kituo cha kuandikisha wapiga kura katika kila gereza kwa Tanzania Bara na chuo cha mafunzo kwa Tanzania Zanzibar.
   (ii) Vituo vilivyoanzishwa chini ya aya ndogo ya (i) vitakuwa ndani ya ngome au uzio wa gereza au chuo cha mafunzo kwa kuzingatia mazingira ya gereza au chuo cha mafunzo husika.
2. Watendaji wa uandikishaji
   (i) Kila kituo cha uandikishaji ndani ya gereza kwa Tanzania Bara na chuo cha mafunzo kwa Tanzania Zanzibar kitakuwa na mwandishi msaidizi mmoja na mwendeshaji wa kifaa cha bayometriki mmoja.
   (ii) Katika kila kituo atakuwepo afisa wa Tume atakayekuwa na jukumu la kuhakikisha taratibu na masharti ya Sheria na Kanuni za uandikishaji zinazingatiwa.
   (iii) Baada ya kupata mapendekezo kutoka Jeshi la Magereza na Chuo cha Mafunzo, Tume itateua Afisa Magereza mmoja kuwa mratibu wa uandikishaji kwa vituo vyote vya magereza kwa Tanzania Bara na Afisa mmoja wa Chuo cha Mafunzo kuwa mratibu wa uandikishaji kwa upande wa Tanzania Zanzibar.
3. Watu wanaoruhusiwa kuingia katika kituo cha uandikishaji ni: -
   (i) mwandishi msaidizi;
   (ii) mwendeshaji wa kifaa cha bayometriki;
   (iii) mfungwa au mwanafunzi wa chuo cha mafunzo anayeomba kuandikishwa au kuboresha taarifa zake;
   (iv) afisa mwandikishaji;
   (v) afisa mwandikishaji msaidizi atakayeidhinishwa na afisa mwandikishaji;
   (vi) Mjumbe wa Tume;
   (vii) Mkurugenzi wa Uchaguzi; na
   (viii) afisa wa Tume.
4. Katika utekelezaji wa majukumu ya uandikishaji, Tume na watendaji wote walioainishwa katika aya ya 3 ya Jedwali hili watapaswa kuzingatia Sheria, Kanuni na Miongozo ya uendeshaji na usimamizi wa magereza na vyuo vya mafunzo.
5. Wapiga kura ambao ni wafungwa au wanafunzi wa vyuo vya mafunzo wanaweza kuboresha taarifa zao katika vituo vilivyoanishwa katika aya ya 1 kwa kuzingatia masharti yaliyoanishwa katika Sheria na Kanuni hizi.
6. Muda wa kufungua kituo cha uandikishaji utakuwa saa mbili kamili asubuhi hadi saa tisa kamili alasiri au kama itakavyoelekezwa na Tume.
7. Watendaji wote wanaoruhusiwa kuingia katika vituo vya uandikishaji vilivyopo katika magereza na vyuo vya mafunzo watapaswa kuwa na utambulisho utakaotolewa na Tume.
8. Kwa madhumuni ya utekelezaji bora wa utaratibu wa uandikishaji wa wafungwa au wanafunzi wa vyuo vya mafunzo na upigaji kura, kutakuwa na mashauriano ya mara kwa mara kati ya Tume na mamlaka zinazohusika na masuala ya magereza na vyuo vya mafunzo.

*Tangazo la Serikali Na. 389 (Linaendelea.)*

9. Elimu ya Mpiga Kura.
Tume itapeleka vipeperushi na nyaraka mbalimbali kwa ajili ya kutoa elimu kuhusu uboreshaji wa Daftari la Kudumu la Wapiga Kura katika magereza na vyuo vya mafunzo.

10. Pamoja na utaratibu huu masharti mengine ya uandikishaji kwa mujibu wa Sheria na Kanuni yatazingatiwa.

Dodoma,
14 Mei, 2024

JACOBS C. M. MWAMBEGELE
*Mwenyekiti wa Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi*

OFISI YA MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI TANZANIA
WELEDI NA UBORA
PROFESSIONALISM & EXCELLENCE
THE OFFICE OF THE ATTORNEY GENERAL TANZANIA